## MIRUNGI

Mirungi ni aina ya mimea inayostawi kwenye hali ya unyevunyevu na milima yenye urefu kati ya futi 4000 hadi 9000. Hapa nchini mimea hii hupatikana kwa wingi kama uoto wa asili katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Hata hivyo kiasi kikubwa cha mirungi itumikayo nchini huingizwa isivyo halali kutoka Kenya.



*Mmea wa Mirungi*

**Mirungi hujulikana kwa majina mengine kama vile:**

- Miraa
- Mbaga
- Mogoka
- Veve
- Bomba
- Kashamba

Mirungi ina kemikali inyojulikana kama *"cathinone"* ambayo humsababishia mtumiaji msisimko, kukosa hamu ya kula na kumfanya kujisikia mwenye furaha.



## MADHARA YA MIRUNGI

Baadhi ya madhara ya Mirungi ni:

- Kukosa hamu ya kula.
- Vidonda vya mdomoni na tumboni.
- Kukosa choo.
- Kupungukiwa maji mwilini.
- Shinikizo la damu.
- Kukosa hamu ya kufanya mapenzi.
- Kupungua kwa nguvu za kiume.
- Mwili kuwasha.
- Maumivu makali ya kichwa.
- Kuharibika kwa ini.

## UTAJIEPUSHAJE NA MATUMIZI YA MIRUNGI?

- Jiepushe na makundi ya watumiaji wa mirungi.
- Shiriki kwenye michezo.
- Jifunze na zingatia stadi za maisha

## SHERIA INASEMAJE KUHUSU MIRUNGI

Kutumia, kuhamasisha matumizi, kuuza, kusafirisha, kuhifadhi au kujihusisha kwa namna yeyote ile na mirungi ni kosa la jinai. Adhabu kwa makosa haya hufikia hadi kifungo cha maisha.

## JUKUMU LA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali unalojukumu la kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kubaini, kutambua na kuthibitisha aina na madhara ya dawa za kulevya.

## KWA USHAURI NA MSAADA:

Nenda kwenye kituo cha ushauri au kituo cha afya kilicho karibu nawe.




*Kwa maelezo zaidi wasiliana na:*
**Mkemia Mkuu wa Serikali**
**Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**
Luthuli/ Barack Obama Drive
S.L.P. 164
**Dar Es Salaam, Tanzania**
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

**Meneja**
**Maabara ya Kanda ya Mashariki**
Luthuli/Barack Obama Drive
S.L.P. 164
**Dar Es Salaam, Tanzania**
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: gcla.east@gcla.go.tz

**Meneja**
**Maabara ya Kanda ya Ziwa,**
Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo
S.L.P. 502,
**Mwanza, Tanzania.**
Simu: +255 28 2500279
Baruapepe: gcla.lake@gcla.go.tz

**Meneja**
**Maabara ya Kanda ya Kaskazini**
Kituo cha Afya Themi
S.L.P. 2095
**Arusha, Tanzania.**
Simu: +255 27 2506394
Nukushi: +255 27 2549026
Baruapepe: gcla.north@gcla.go.tz

**Meneja**
**Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya
New Forest Area
S.L.P. 2875
**Mbeya ,Tanzania.**
Simu: +255 25 2502311
Nukushi: +25525 250 312
Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

**Meneja**
**Maabara ya Kanda ya Kusini**
Ushirika House
Barabara ya TANU
S.L.P. 1414
**Mtwara,Tanzania.**
Simu: +255 23 233 4760
Nukushi: +255 23 233 4761
Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI**

ISO 9001:2008
ISO 17025:2005

## IDARA YA SAYANSI JINAI NA HUDUMA ZA VINASABA

# IFAHAMU MIRUNGI NA MADHARA YAKE



**KITENGO CHA SAYANSI JINAI – KEMIA (FORENSIC CHEMISTRY)**